**Majukumu ya Msingi ya Maktaba katika Kuleta Mabadiliko kwenye Sekta ya Elimu Nchini Tanzania: Uchunguzi Yakinifu**

**Imewasilishwa**
**Na**
**Goodluck Mosha**
**Mkutubi**
**Chuo Kikuu Mzumbe**

**Kwenye Kongamano la Pili la Kitaifa la Huduma za Maktaba, Tamasha la Vitabu na Usomaji.**

**Mada: Mchango wa Huduma za Maktaba, Utunzaji wa Nyaraka na Mafunzo ya Ukutubi katika Uboreshaji wa Elimu Tanzania**

**Tarehe 23 -24 Novemba 2022, Ukumbi: Tanga Beach Resort and Spa ♨**

## Utangulizi

Sekta ya elimu ni nguzo na msingi katika uchumi wa taifa. Katika jamii ya kisasa elimu ni chombo cha uhakika cha mabadiliko, kuwapa nguvu, kukomboa, na kuboresha maisha ya watu (Adegoke, Fijabi, na Bamidele, 2014). Elimu ni urithi bora ambao nchi inaweza kuwapa raia wake. Igbuzor (2006) anabainisha kwamba elimu ni mahitaji ya msingi na ni haki kila mwanadamu aipate.

## Maktaba katika Ulimwengu wa Elimu

Elimu na Maktaba ni dhana mbili ambazo haziwezi kutenganishwa na hazigawanyiki kwa sababu vyote viwili kimsingi vinashikamana na kushabihiana na mara zote huishi pamoja. Katika Taasisi za Elimu ya Juu, maktaba zinathaminiwa sana na huchukuliwa kama gurudumu la taasisi hizo kama inavyoshadidiwa na Adegoke, Fijabi & Bamidele (2014) kwa kuweka wazi kwamba, kikategoria hakuna taasisi ya kielimu inayoweza kuishi na kuendelea bila kuwa na maktaba iliyopangiliwa vizuri. ( Kuanzia elimu ya msingi hadi vyuo vya elimu vya kati na ya juu, maktaba zitaendelea kuwa chombo cha msingi cha mfumo wa elimu. Kwa hiyo, inaweza kusemwa kuwa maktaba ni mojawapo ya maeneo ambayo yakifanyiwa mapinduzi chanya yanaweza kuleta mabadiliko mazuri katika mfumo wetu wa elimu. Maktaba zinaweza kutazamwa kama "moyo" wa chuo kikuu au taasisi yoyote ya elimu. Hii inaonesha kuwa maktaba nzuri zinaonekana kama kiungo muhimu cha mpango na mkakati wowote wa kielimu.

Utafiti wa Simba (2019) unasisitiza kwamba ukiachilia mbali aina ya maktaba, maktaba ni neva kuu za mchakato wa kujisomea; zina ushawishi wenye nguvu katika kusisimua hamu ya kusoma na kuimarisha utafiti na ujuzi wa fikra tunduizi kwa wanafunzi. Kwa upande mwingine, Ntulo na Nawe (2008) wanaona maktaba ni kama maabara; kama ambavyo mwanafunzi wa sayansi hawezi kujifunzia sayansi katika mazingira yasiyokuwa na maabara vivyo hivyo mwanafunzi hawezi kujifunza, kusoma, na kufaulu vizuri asipotumia maktaba. Hii inafanana na wazo la Mgina na Lwehabura (2012) ambao wanasema kuwa kuna uhusiano mkubwa kati ya kufanya vizuri kimasomo kwa mwanafunzi na uwepo wa maktaba nzuri katika mazingira yake ya kujifunzia.

Mwongozo wa Viwango na Sheria ya Elimu ya Vyuo Vikuu Tanzania (2019) unagusia dhima ya maktaba katika elimu ya chuo kikuu, na sehemu ya 6.7 imeweka viwango vya maktaba ya chuo kikuu. Kinyume na viwango hivi, chuo hakitasajiliwa kikamilifu na Mamlaka ya Usimamizi wa Vyuo Vikuu Tanzania (TCU). Katika taasisi nyingine za elimu Tanzania kama vile shule, maktaba ni hitaji la lazima kwa ajili ya usajili lakini nyingi zimesajiliwa na zinaendeshwa bila maktaba.

**Maktaba za Vijijini na Mpango wa Elimu ya Watu Wazima Nchini Tanzania**

Kampeni za kisomo nchini Tanzania mwanzoni mwa miaka ya 1970 zilitambua umuhimu wa hitaji la matini zilizochapishwa ili kufuta ujinga, na kwa mwitikio wa hilo hitaji, maktaba kadhaa zilianzishwa. Tanzania ilikuwa na maktaba za vijiji takribani 3,000 zenye makala 400 katika kila kijiji (Olden, 2005). Maktaba kama hizi zilisaidia Mpango wa Elimu ya Watu Wazima kuhakikisha kuwa wahitimu wa Elimu ya Watu Wazima wasimalize shule yao bila kujua kusoma na kuandika kutokana na ukosefu wa matini za kusoma. Mpango wa Elimu ya Watu Wazima ukisaidiana na Maktaba ya Taifa ulifanya kiwango cha wasomi nchini kupanda kufikia kwenye 90% kwenye mwaka 1980, na takwimu hizi zilikuwa kati ya takwimu za juu duniani. Kwa hivi sasa, haijulikani ni maktaba ngapi za vijijini ambazo bado zinafanya kazi nchini Tanzania. Tangu mwanzoni mwa miaka ya 1990 kiwango cha kuweza Kusoma, Kuandika, na Kuhesabu (3 K) kimeshuka kwa kiasi kikubwa. Kiwango cha sasa cha ujinga ni 22.4 % ambayo ina maana wakazi wapatao milioni 5.5 wenye umri wa miaka zaidi ya 15 hawawezi kusoma, kuandika na kuhesabu kwa ufasaha. Serikali ya Tanzania ilizindua Elimu ya Watu Wazima Kitaifa na Mkakati wa Elimu kwa Umma wa mwaka 2020/21 hadi 2024/25. Mpango huu unajumuisha kufufua kozi za Elimu ya Watu Wazima nchi nzima. Lengo la mkakati huu ni kuhakikisha kuwa maktaba moja ya vijijini katika kila mkoa ina vitabu vya kutosha vinavyolingana na mahitaji ya watu wazima ifikapo mwaka 2025, na kuhakikisha kwamba Maktaba Jogefu/Tembezi (Mobile Library) imeanzishwa katika jamii zinazohamahama ifikapo 2025 (URT, 2020).

**Huduma ya Maktaba katika Shule za Tanzania**

Huduma ya maktaba shuleni ilipatiwa fedha na TLS kwa kutumia fedha za serikali. Hii ilisababisha kuanzishwa kwa Huduma ya Maktaba Shuleni (SLS), iliyokuwa na makao makuu katika Maktaba Kuu ya Taifa Dar es Salaam na ilipatiwa fedha katika Mpango wa Maendeleo wa 2 na wa miaka 5 mwaka 1969-1974. Vilevile; Shirika la Elimu, Sayansi na Utamaduni la Umoja wa Mataifa (UNESCO) lilitoa msaada hasa kwa wafanyakazi wa kwanza. Huduma ya Maktaba inayotembea ilianza mwaka 1971. Vitabu vilitolewa shuleni mara mbili au tatu kwa mwaka katika mikoa mitatu, hii iliruhusu walimu kuchagua vitabu vinavyofaa katika shule zao (Ilomo, 1985). Katika kipindi hicho, wanafunzi wote waliomaliza darasa la saba walikuwa na uwezo wa kusoma, kuandika, na kufanya hesabu zilizo katika kiwango chao cha elimu.

Hadi mwaka 1976, Huduma ya Maktaba za Shule (SLS) iliendeshwa na mtaalamu mmoja na Mkutubi Msaidizi mmoja. Upanuzi wa Huduma ya Maktaba Shuleni ulisimama mwaka 1976. Katika Mpango wa Maendeleo wa 3 wa miaka 5 wa mwaka 1976-1981, hakukuwa na mpango wowote na hakuna chochote kilichofanyika. Hakuna tena maktaba za mifano zilizofunguliwa (mpango ulikuwa

kufungua maktaba moja katika kila mkoa katika mikoa 20 ya Tanzania) na hakukuwa tena na mikoa iliyohudumiwa na maktaba zinazotembea. Hii inaweza kuwa sababu moja kuu ya kushuka kiwango cha usomi Tanzania; kwa sababu kama ilivyobainishwa mwanzo kwamba makataba ni moyo wa elimu, na kwa kuwa moyo haufanyi kazi vema na elimu haiwezi kustawi kamwe.

## Dhima ya Maktaba katika Kuibadili Sekta ya Elimu

Maktaba zinategemewa zijiweke katika nafasi ya kuwezesha elimu endelevu na kueneza stadi za maisha, kazi, na maendeleo ya kudumu. Kitabu cha UNESCO cha Sera za Kujisomea katika Maisha kwa Muda Mrefu (Lifelong Learning) kinaeleza kuwa maktaba ziwe sehemu ya muunganiko wa jamii, na mahali pa kukutania panapotengeneza mahusiano kati ya watu na taasisi ambazo ni mojawapo ya sehemu zinzazoinua kujisomea maisha yote (Ouane, 2009). Utafiti wa Haggstrom (2004) unaongezea kuwa, Maktaba za Umma (Public Libraries) zitakuwa mahali pa kuunganisha mafunzo ya wenyeji – hata kama ni rasmi au sio rasmi kwa kutoa mwongozo na mafunzo na ya namna ya kutafuta na kutumia haya maarifa na kuweka kiwango cha viini vya maarifa.

Katika chuo kikuu na taasisi nyingine za elimu, maktaba huwa na dhima lukuki kwa mafanikio ya taasisi kimsingi pamoja na utume na maono yao. Hii hukamilika kwa kuhakikisha wanafunzi wanapata taarifa halisi wanazohitaji ambayo inabadilishwa kuwa maarifa. Magut na Kiplagat (2022) wanasisitiza kwamba bila maktaba; kujifunza kupitia mtandao na kujifunza kwa elimu ya umbali inayotolewa na vyuo vikuu itashindikana. Wataalamu wa maktaba husaidia watumiaji wa umri wowote kuendeleza digitali, vyombo vya habari, na taarifa ya ujuzi wa kusoma na kuandika, ambao ni muhimu kwa mafanikio ya matumizi, kuunda, na kushirikiana katika kupeana maarifa.

Maktaba ni taasisi zinazofungua mafanikio ya kujua kusoma na kuandika ulimwenguni. Katika ilani ya UNESCO/IFLA ya Maktaba za Umma (1994) imeelezwa kwa tume muhimu zinazohusiana na maarifa, kisomo, elimu na utamaduni ziko katika msingi wa huduma ya maktaba ya watu wote.

## Dhima ya Maktaba katika Kuibadilisha Elimu

Leo dhima ya maktaba na wataalamu wa maktabani imebadilika duniani kote. Wao kwa sasa hivi sio wawekaji na watunzaji wa vitabu; bali, wanabadilika kuwa wawezeshaji wa nafasi za taarifa na kujisomea endelevu maishani na msisitizo kwenye huduma: wakitambua mahitaji ya watumiaji, na ufumbuzi katika kuwasiliana.

Maktaba ni muhimu kwa kila mkakati wa muda mrefu wa kisomo cha watu wazima, elimu, kutoa taarifa, na uchumi, utamaduni na maendeleo ya kijamii. Imejionesha kuwa wakutubi na waelimishaji watakapoungana kufanya kazi pamoja, wanafunzi watapata mafanikio ya kiwango cha juu cha kisomo, kusoma, kujifunza, utatuzi wa matatizo, ujuzi na maboresho katika TEHAMA. Zifuatazo ni dhima zinazoikabili maktaba ambazo zikitumiwa vema zitaleta mabadiliko ya kielimu Tanzania:

a) Maktaba zitoe dhima muhimu za kutangaza na kuubadilisha mfumo wa elimu. Sio rahisi kwa nchi yoyote au jamii kustawi bila kuungwa mkono kikamilifu na mfumo wa elimu. Hitaji la msingi katika kuubadli mfumo wa elimu ni maarifa ambayo yamechaguliwa, kuhifadhiwa, kuchakatwa, na kusambazwana maktaba.
b) Maktaba zinatakiwa zitoe mwanya kwa taarifa za mtaala na maendeleo kiujuzi na vifaa. Pia, zitoe nafasi ya kupanga, kutekeleza na kutathmini programu za mafunzo zenye muunganiko na viini vya taarifa.
c) Wakutubi kama wataalamu wanatakiwa watangaze elimu endelevu kimaisha; wao ni wadau muhimu wa waelimishaji na viongozi wa kuwasaidia wanafunzi kutafuta matini sahihi za kusoma. Wakutubi kama wakala wa mabadiliko wanapaswa kutumia teknolojia kuwasaidia wanafunzi kutumia teknolojia kama hizo kupata matini popote kwa saa 24/7.
d) Maktaba zinapaswa kuwa moyo wa mabadiliko yatakayokuwa ya lazima kuifanya elimu iwe ya ulimwengu yenye kuleta athari chanya na yenye maana kwa wote.
e) Maktaba ni waunga mkono wakuu katika mabadiliko kutoka kujifunza uso-kwa-uso hadi kujifunza kupitia programu za mtandaoni. Hii ni kwa vile wanafunzi wengi wanavyochukua kozi za mtandaoni, maktaba zinapaswa zitoe uwezekano wa kupata matini za kusoma vijijini ambayo itasaidia elimu kubadilika kidigitali.
f) Maktaba na wakutubi wanapaswa waandae programu zitakazowafikia walio mbali hasa za makundi maalumu ya watu wenye ufinyu wa stadi za elimu.
g) Maktaba na wakutubi wanapaswa kuwa wadau katika elimu, hasa wakati wa kuandaa mitaala, na wanatakiwa kuingiza rasilimali katika vifaa vya kufundishia na kujifunzia.
h) Wanatakiwa wawapatie waelimishaji vifaa na taarifa zinazofaa za maendeleo ya kitaalamu kwenye vifaa kutoka ndani na nje ya mfumo wa elimu.
i) Maktaba zinapaswa kuwataarifu wanafunzi kwa kuwapatia taarifa za sasa bila vizuizi katika nakala ngumu na mifumo ya kielektroniki. Kuwa

na uwazi katika sehemu zote za shughuli za kiuchumi ni kichocheo cha kuendeleza uchumi wenye maarifa ya kutosha.

j) Maktaba za shule lazima ziwapatie wanafunzi na walimu uwezekano wa kupata viini mbalimbali vya rasilimali kama vile matini zilizochapishwa na za kusikiliza na kuona vitakavyowasaidia kuwa na usawa katika matumizi ya nafasi.

k) Maktaba zinafanya kazi pamoja na taasisi za kielimu katika kutekeleza programu za kujifunza mtandaoni na mbali, kwa kuwapa watumiaji taarifa wanazohitaji kupitia mtandao, tovuti, video, ukurufunzi, runinga, mitandao ya kijamii, blogu, n.k.

l) Kukua kwa Elimu ya Kielektroniki/Elimu Kimtandao (e-learning) ambayo imeitwa maktaba ya kujifunzia imesababisha wakutubi kushirikiana na wanazuoni kuunda programu za aina hii na kuzitekeleza.

**Changamoto**

Maktaba nchini Tanzania zimeshindwa kushiriki kikamilifu katika kuunga mkono mabadiliko ya kielimu kwa sababu:

- Hazina wakutubi wa kutosha na wenye utaalamu wa TEHAMA, wenye ujuzi na utaalamu katika kujifunza, kufundisha, kutumia taarifa, na kuzalisha kwenye mtandao, kwa ujumla ushiriki wao katika mtandao hauwezi kuonekana.
- Maktaba za umma, za shule, na za vyuo vikuu ni wahanga wa bajeti pungufu. Kwa kuzingatia hali ya uchumi ya sasa, maktaba zinakabiliana na upungufu wa fedha ambao una madhara makubwa katika dhima za maktaba katika sekta ya elimu. Swali linaloulizwa ni "vipi maktaba zitatoa uwazi wa taarifa zinazotakiwa na wasomaji wakati gharama hazikamatiki ziko juu sana?"
- Nchini Tanzania, shule nyingi za msingi na sekondari hazina maktaba. Ofisi za walimu wakuu pia hutumika kuhifadhi baadhi ya vitabu vya kiada vichache na vya walimu vya rejea.
- Maktaba zetu, hasa za umma, zina vitabu vya zamani na matini zisizoendana au zitakazoweza kuleta mabadiliko katika sekta ya elimu.
- Ukosefu wa viwango vya maktaba za umma na za shule: viwango vya maktaba ni miongozo ya namna maktaba za kielimu, ziwe za vyuo vikuu, vyuo vya kati, lazima zitumike, zipangiliwe na kuboreshwa. Viwango vya maktaba ni vipimo vya kutathimini utendaji wa maktaba au ni maktaba zipi zinazoweza kusemwa ni nzuri au mbaya.

- Katika shule, kuna kutokuelewa kwa walimu na wanafunzi kuhusu dhima ya maktaba ya shule na hivyo kuongeza ufinyu wa kuitumia maktaba ipasavyo hata kama imepangiliwa vizuri.
- Teknolojia na mtandao vimekuwa na msukumo mkubwa kwenye maktaba na namna zinavyotoa huduma. Taarifa za kidigitali zinazokua kwa haraka zimeathiri utendaji na mifumo katika maktaba kwa muda mfupi sana, matokeo yake zimeacha mianya ya ujuzi unaohitajika katika kuendesha maktaba za kidigitali.
- Mabadiliko ya uchapishaji wa kisomi yameeleza upya dhima za wakutubi, kwenda mbali kuliko muda wa maudhui. Wakati hii ikitokea, wakutubi wanaona changamoto kuelezea thamani ya kazi yao katika majimbo yao.
- Tanzania haina sera ya taifa juu ya maendeleo ya maktaba ambayo inaathiri ile nia ya dhati ya kuendeleza maktaba za aina yoyote, isipokuwa za vyuo vikuu.

**Mapendekezo**

Kutokana na mitazamo iliyotangulia mapendekezo yafuatayo yametolewa:

- Ili kuboresha elimu nchini, huduma ya maktaba shuleni ambayo imepuuzwa siku nyingi ipewe kipaumbele. Ujenzi wa madarasa mapya na kufunguliwa kwa shule mpya uende sambamba na ujenzi wa maktaba za kisasa zenye vitabu vya kutosha, vifaa, na wakutubi wawepo.
- Mtaala wa vyuo vya ualimu Tanzania lazima ujumuishe kozi ya maktaba ili wawapo shuleni kama hakuna mkutubi wasaidie katika kusimamia maktaba ya shule, pia wawape wanafunzi ujuzi wa msingi wa maktaba.
- Serikali ya Tanzania inapaswa kurudi, kuimarisha au kutekeleza sheria ya kuhakikisha kila shule inayosajiliwa sharti iwe na maktaba. Pia ziwe na wakutubi wenye taaluma ya ukutubi.
- Kuna haja ya kuweka misingi ya maktaba za shule za serikali. Shukurani za pekee ziiendee TCU ambayo imeweka viwango vya maktaba za vyuo vikuu nchini Tanzania.
- Kama Tanzania inaridhia kutoa uwazi kwa matini za kusoma za kisasa zinazoenda na wakati katika shule na vyuo vya kati, tunashauri Wizara ya Elimu iweke bajeti ya kuweza kupata Vitabu vya Kielektroniki (eBooks) na Majarida ya Kielektroniki (eJournals). Kinyume na hali

ilivyo sasa ambapo ni vyuo vichache vinavyoingia kupitia Muungano wa Maktaba za Vyuo Vikuu na Taasisi za Utafiti Tanzania COTUL.

- Maktaba zitengewe bajeti ya kutosha kama zinatakiwa ziwe na tija na zenye kuvutia. Maktaba ziwe sehemu muhimu ya sera ya muda mrefu ya mpango wa elimu ikiwa na kisomo, utoaji taarifa na kujisomea endelevu.
- Maktaba lazima zishirikiane na wadau wengine na wachapishaji wa ndani.
- Maktaba ambazo zinahifadhi ya vifaa vya kutosha na utunzaji itasaidia walimu madarasani na kutoa elimu ya nadharia ya shughuli za maabara.
- Kama maktaba zitaingizwa ndani ya mfumo wa elimu ya Tanzania itasaidia kujenga moyo wa kujitambua katika masomo ambayo itaboresha maendeleo kuhusu kiu ya elimu endelevu.
- Umoja wa Maktaba Tanzania "Tanzania Library Association" bila kuchelewa itoe viwango vya maktaba za shule kuhusu majengo, samani, vifaa, watumishi wa akiba na huduma.

**Wakati tunapoangalia kuhusu maktaba za wakati ujao Tanzania tutegemee kuona...**

- Maktaba ikiwa kiini cha uvumbuzi wa maarifa na kupatia maarifa.
- Maktaba iwe mahali muhimu pa watu wote, mahali popote na katika kifaa chochote.
- Zijenge ushirikiano wa kawaida kati ya wataalamu wa TEHAMA na wakutubi katika kutumia teknolojia zinazojitokeza.
- Zitumie mitandao ya kijamii kama jukwaa la wanafunzi kupatia taarifa na kutumia maktaba kama mahali pa kawaida pa kujifunzia.
- Maktaba zishirikishwe kwenye kila badiliko la kielimu linalofanyika Tanzania.
- Maktaba katika taasisi za kielimu zishirikiane na idara na makundi yanayohusika na kujifunza mtandaoni (TEHAMA, Vituo vya kufundishia na kujifunzia, n.k.,) kuiingiza huduma za maktaba kwa uhakika katika maisha ya mwanafunzi.
- Maktaba na wakutubi wafanye bidii ya kuwaelewa walezi wao kwa kina, mahitaji, na tabia ili kuendeleza huduma inayolengwa.
- Kuwahudumia wanafunzi wa mtandaoni ionekane kama kazi ya kila mkutubi.

## Hitimisho

Matumizi ya maktaba yanaweza kuhisiwa na kujumuishwa mara moja, hasa tunapoangalia hali ya elimu ya watu maskini. Maktaba lazima zitoe vitabu vinavyofaa na matini nyingine karibu sawa na bure ili watoto wa maskini na matajiri wapate fursa sawa kutokana na huduma hii ya bure itakayosaidia wasome na kupata elimu bora.

Maktaba ni taasisi muhimu ambazo haziwezi kutenganishwa na elimu. Uwepo wa maktaba hauepukiki katika elimu ya taifa. Kwa hiyo, kila kinachofanywa kuboresha elimu kinafanywa kuboresha taifa. Kukosekana kwa maktaba kutakuwa na athari hasi kwenye elimu.

Watekelezaji wa sera ya elimu inapendekezwa waurudishe mfumo mahali panapostahili kuimarisha uanzishwaji na maendeleo bora ya maktaba za kila shule ya sekondari kama chombo cha kuhakiki utoaji wa elimu.

## References


Adegoke, O., Fijabi, N.M., & Bamidele, I.A. (2014). The role of the library in the transformation of the educational system in Nigeria. Akoka Journal of Education, 6(2), 53-62.

Benard, R., & Dulle, F. W. (2014). Assessment of access and use of school library information resources by secondary school students in Morogoro municipality, Tanzania.

Haggstrom, B. M. (2004). The Role of Libraries in Lifelong Learning. Final Report of the IFLA Project under the Section for Public Libraries. *International Federation of Library Associations and Institutions (NJ1).*

Igbuzor, O. (2006). The state of education in Nigeria. *Economic and Policy Review*, *12*(3).

Ilomo, C. S. (1985) *Towards more effective school library programmes in Tanzania.* Dar es Salaam: Tanzania Library Services. 6p. (Occasional Papers; no. 23)

Kaungamno, E. E. (1972). A national plan for the development of library services.

Kaungamno, E. E. and C. S. Ilomo. (1979) *Books build nations, vol. 2: Library services in Tanzania.* London: Transafrica; Dar es Salaam: Tanzania Library Services: 194-197.

Krolak, L. (2006). The role of libraries in the creation of literate environments. *International Journal of Adult and Lifelong Education*, *4*(1/4), 5.

Magut, H. J., & Kiplagat, S.(2022) Covid-19 Pandemic and The Role of Kenyan University Libraries in Online Education. *International Journal of Innovative Science and Research Technology*

Mgina, S., & Lwehabura, M. J. (2011). Status of Secondary School Libraries under the Secondary Education Development Plan: A Case Study of Dodoma Municipality, Tanzania. *African Journal of Library, Archives & Information Science*, *21*(2), 167.

Mubofu, C., & Malekani, A. (2019). Challenges of school libraries and quality education in Tanzania: A review.

Ntulo, G., & Nawe, J. (2008). Secondary Education Development Plan (SEDP) and the provision of library service in Tanzania: a Case Study of Sumbawanga Municipality. *University of Dar es Salaam Library Journal*, *10*(1-2).

Olden, A. (2005). “For poor nations a library service is vital”: Establishing a national public library service in Tanzania in the 1960s. *The Library Quarterly*, *75*(4), 421-445.

Ouane, A. (2009). UNESCO’s drive for lifelong learning. In *The Routledge international handbook of lifelong learning* (pp. 332-341). Routledge.

Simba, C. A. (2014). *School library resource centres in Iringa and Njombe regions of Tanzania: their status and role in resource-based learning* (Doctoral dissertation).

TCU (2022).Handbook for standards and guidelines for university education in Tanzania

URT (2020) National Adult Literacy and Mass Education Rolling Strategy 2020/2021-2024/25